VERMONT
DEPARTMENT OF LABOR

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA: MSAADA WA JANGA LA UKOSEFU WA AJIRA

## MASWALI YA KIUJUMLA KUHUSU MSAADA WA JANGA LA UKOSEFU WA AJIRA (PUA)

**Najaribu kuwapigia lain ya msaada, hata hivyo hainiruhusu kusubirishwa, huwa inakata tu. Ninawezaje kuendelea?**

Ikiwa unapigia lain ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira na unapata ujumbe kuwa wajumbe wote wana shughuli, hali hiyo husababishwa na lain kuwa bizi, na foleni kujaa. Tafadhali soma kipengele chenye maswali yanayoulizwa mara kwa mara, ili kusaidia kusuluhisha maswali kabla ya kupiga simu tena.

**Ina maana gani ikiwa sina sifa za ukosefu wa ajira wa kawaida, lakini taarifa zangu hazipo kwenye Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira bado?**

Ikiwa hauna sifa za ukosefu wa ajira wa kawaida, maombi yako yatapitiwa na Idara ili kuhakiki ustahiki wako wa Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Baada ya uhakiki kufanyika, utapokea taarifa kutoka kwa Idara yenye kukutaarifu kuhusu ustahiki wako. Ikiwa una sifa, utaweza kumaliza kujaza maombi yako ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira na kuanza kuweka thibitisho za dai zako za wiki.

**Ni wakati gani ninaweza kutuma maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Ni sharti utume kwanza maombi ya mafao ya bima ya ukosefu wa ajira wa kawaida ili kuweza kutambua kama una sifa za kupata mafao ya ukosefu wa ajira wa kawaida ama mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu

wa Ajira. Ikiwa bado haujatuma maombi ya ukosefu wa ajira wa kawaida, ingia https://vermont.force.com/DOLClaim/s/. Kulingana na uwasilishaji wako wa maombi, unaweza kuongozwa mara moja kumaliza maombi yako ya dai la Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Kama hutoongozwa mara moja kufanya hivyo, itakubidi kusubiri DOL ipitie ombi lako. Utapewa taarifa, punde uamuzi utakapofanyika.

**Nimehafifisha mafao yangu ya kawaida ya UI, je nitume maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira ama nifanye nini?**

Ikiwa umehafifisha wiki zako 26 za mafao ya bima ya ukosefu wa ajira wa kawaida na unajaribu kuanza kutumia wiki 13 za nyongeza za Msaada wa Dharura ya Janga la Ukosefu wa Ajira (PEUC), hautakiwi kujaribu kutuma maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Uwezekano ni kuwa, utapokea ujumbe wa hitilafu ikiwa utajaribu kutuma maombi kwani teyari umekwisha weka dai la ukosefu wa ajira. Hakuna chochote unahitaji kufanya hadi pale programu ya PEUC itakapotekelezwa.

**Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira utajumuisha wiki zipi?**

Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira itatoa mbadala wa mshahara kwa wadai wenye sifa, utajumuisha kwanzia wiki ya Machi 15, 2020, kipindi oda ya utendaji ya Gavana Scott ilipoanza kutekelezwa.

**Itakuwaje ikiwa dai langu la mafao ya kawaida ya UI limekataliwa na ninapata ujumbe wa hitilafu kila ninapojaribu kuendelea kutuma maombi ya mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Ikiwa ulikataliwa mafao ya ukosefu wa ajira wa kawaida, hili halitoathiri sifa zako za kupata mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Maombi yako yapo katika ukaguzi, na Idara ya Wafanyakazi itakutaarifu kama una sifa za kutuma maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Ninapojaribu kumaliza maombi yangu ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira, huwa ninaambiwa kuwa rekodi zangu hazipo na kwamba ninatakiwa kumaliza maombi ya ukosefu wa ajira wa kawaida. Na nikijaribu kamaliza maombi ya ukosefu wa ajira wa kawaida, ninaambiwa teyari ombi lipo. Nifanyeje?**

Ikiwa umefuata hatua zote za utumaji maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira (ikiwa ni pamoja na kujaza kwanza maombi ya awali ya ukosefu wa ajira) na unapokea ujumbe wa hitilafu unapojaribu kuhakiki taarifa zao kwenye Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira, hii inamaanisha kuwa maombi yako ya UI yanahitaji kufanyiwa ukaguzi zaidi na Idara. Hautaweza kumaliza maombi yako ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira, hadi pale ukaguzi huo utakapokamilika. Idara itakutaarifu kuhusu ustahiki wako.

**Dai langu liko kwenye Uamuzi. Hii ina maana gani?**

Kama dai lako liko kwenye uamuzi, kutakuwa na jambo kwenye dai lako ambalo Idara inahitaji kulifanyia utafiti zaidi. Mchakato huu unaanzishwa kwa msingi wa majibu uliyotoa katika maombi yako ya awali ya ukosefu wa ajira. Dai lako litachakatuliwa kwa mujibu wa namna lilivyopokelewa.

**Ninarudi kazini. Je, nitapaswa kufanya chochote kuwataarifu Idara ya Wafanyakazi?**

Ikiwa unarudi kazini, hautohitaji kuwataarifu Idara wakati huu. Utapaswa tu kuacha kuweka madai yako ya wiki. Ikiwa utaweka madai ya wiki huku ukiwa umeajiriwa kikamilifu, hilo litakuwa tendo la udanganyifu na utakoseshwa mafao yako. Kama unafanya kazi ambayo unaweka madai ya mafao ya UI, utapaswa kuripoti masaa ambayo umefanya kazi na mshahara uliopata.

# SIFA ZA KUPATA MSAADA WA JANGA LA UKOSEFU WA AJIRA

**Ninajuaje kama nina sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Ikiwa wewe ni kontrakta binafsi, umejiajiri, umenyimwa ama huna sifa za kupata mafao ya ukosefu wa ajira wa kawaida au FPEUC (programu nyongeza ya mafao), unaweza kuwa na sifa za kupata mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Hali zipi zinanifanya nisiwe na sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Ikiwa unaweza kufanya kazi nje ya ofisi na kulipwa ama unapokea likizo ya malipo ya ugonjwa ama likizo nyingine yoyote ya malipo, hautakuwa na stahiki ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Ninahitaji kuwa na kipato cha pesa kiasi gani, ili niwe na sifa ya kupata mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Unapaswa kuwa na kipato cha angalau $2,871 kwenye msingi wa kipindi cha malipo ya juu ya robo awamu. Kwenye robo tatu nyingine za awamu, unapaswa kupata kipato cha angalau asilimia 40 ya kipato ulichopata kwenye robo awamu ya malipo ya juu zaidi. Vinginevyo, utakuwa na sifa ya kupata kiasi kidogo cha mafao.

***ZAIDI KUHUSU WALIOJIAJIRI***

**Ninajuaje kama nimejiajiri?**

Miongozo ya serikali ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira inawatambua watu “waliojiajiri” kuwa wale ambao msingi wa utegemezi wao wa kipato upo katika utendaji wa huduma zilizopo kwenye biashara zao binafsi. Hii inawajumuisha pia makontrakta binafsi pamoja na wengineo.

**Nimejiajiri sasa, lakini nilifanya kazi kwa mwajiri wangu mwaka 2019. Ninaomba maombi wapi?**

Ikiwa ulipata kipato cha angalau $4,025 kwenye kalenda ya mwaka 2019 kutoka kwa mwajiri (ama waajiri) ambao waliondoa kodi kutoka kwenye cheki yako ya malipo, unaweza kuwa na sifa ya kupata mafao ya ukosefu wa ajira wa kawaida. Hatua ya kwanza katika kutambua ustahiki wako ni kumaliza maombi ya awali ya ukosefu wa ajira ambayo yataazimia kama una sifa za bima ya ukosefu wa ajira ama Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Kama ninaishi Vermont na nimejiajiri kwenye jimbo jingine, wapi ninapaswa kutuma maombi ya mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Unapaswa kutuma maombi kwenye jimbo ambalo ulikuwa unafanya kazi kipindi ulipokosa ajira, ulipokosa ajira kwa sehemu, ama kushindwa kufanya kazi kutokana na sababu zinazohusiana na COVID-19 zilizoorodheshwa kwenye kipengele cha 2102(a)(3)(A)(ii)(I) cha sheria ya CARES. Ikiwa ulifanya kazi kwenye zaidi ya jimbo moja katika kipindi hiki, basi unaweza kutuma maombi kwenye jimbo lolote kati ya hayo.

**Ninapata sehemu kubwa ya mapato yangu kutoka kwenye ajira yangu ya wakati-wote, lakini pia ninamiliki biashara yangu binafsi. Je, nitachukuliwa kama mtu aliyejiajiri katika maazimio ya mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Hapana. Miongozo ya serikali ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira yanamtafsiri mtu kuwa aliyejiajiri pale kipato cha msingi cha mtu huyo kinapotokana na huduma zilizopo kwenye biashara binafsi za mtu huyo.

*VISA VYA USTAHIKI*

**Je, nina sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira ikiwa sijawahi kufanya kazi hapo mwanzo ama muda mrefu umepita tangu nimefanya kazi mara ya mwisho?**

Unaweza kuwa na sifa za Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira kama:

- Ulipangiwa kuanza kufanya kazi na huna kazi kwa sasa ama huwezi kuanza kazi hiyo kutokana na COVID-19
- Ofa yako ya kazi ilisimamishwa kwasababu ya COVID-19
- Umekuwa mtoa riziki ama msaidizi mkuu wa familia kwasababu kiongozi wa familia amefariki kutokana na matokeo ya moja kwa moja ya COVID-19

**Mimi ni mfugaji wa ng'ombe za maziwa. Je, nina sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Ndio, wakulima wana uwezekano wa kuwa na sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira na wanapaswa kuanza kwa kuwasilisha maombi ya awali ya ukosefu wa ajira.

**Je, nina sifa za kupata Msaada Wa Janga La Ukosefu Wa Ajira ikiwa ajira yangu inaniruhusu kufanya kazi nje ya ofisi na kulipwa?**

Hapana. Kama unafanya kazi nje ya ofisi na unalipwa na mwajiri wako, hautakuwa na sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Je, nina sifa za kupata mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira ikiwa sifanyi kazi lakini ninapokea likizo ya malipo ya ugonjwa ama aina nyingine ya likizo ya malipo kutoka kwa mwajiri wangu?**

Unaweza. Ikiwa unapokea malipo kwa sehemu ya likizo ya ugonjwa, unaweza kuwa na sifa ya kupata kiasi cha wiki kilichopunguzwa cha mafao (WBA). Ikiwa kiasi chako cha likizo ya malipo ni kikubwa kuliko kiasi cha wiki cha mafao (WBA), hautokuwa na sifa.

**Je, ninaweza kupokea mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira kama bado ninafanya kazi ila masaa yangu yamepunguzwa?**
Ikiwa unafanya kazi masaa machache kutokana na COVID-19 na hivyo umepoteza kipato, utapaswa kutuma maombi ya mafao ya bima ya ukosefu wa ajira. Ustahiki wako wa ukosefu wa ajira wa kawaida ama Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira utaamuliwa baada ya wewe kutuma maombi.

**Nilifanya kazi wakati wote na nikaachishwa kazi. Lakini, ninamiliki pia biashara ya pembeni ambayo imefungwa kutokana na COVID-19, je nina sifa za Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**
Ikiwa umeachishwa kazi kutoka kwenye ajira ya wakati wote, unauwezekano wa kuwa na sifa ya ukosefu wa ajira wa kawaida. Ikiwa teyari unakusanya mafao ya ukosefu wa ajira wa kawaida, hautoweza kutuma maombi ama kupokea mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira juu ya mafao hayo.

**Ikiwa nipo kwenye likizo ya malipo ya matibabu iliyothibitishwa na mwajiri wangu, na sina sifa za ukosefu wa ajira wa nchi kutokana na kutoweza ama kutokuwa na nafasi ya kufanya kazi, je nitakuwa na sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**
Inategemea. Kama likizo hiyo ya matibabu inatokana na sababu zinazohusiana na COVID-19 ambazo zimeorodheshwa kwenye kipengele cha 2102(a)(3)(A)(ii)(I) cha sheria ya CARES, utaweza kuwa na sifa ya kupata mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Ikiwa hali yako si moja ya sababu zinazohusiana na COVID-19 na hauwezi kufanya kazi ama kuwepo kazini kutokana na sababu zinginezo, hautakuwa na sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu la Ajira.

*KUTOKUWA NA SIFA*

**Nilituma maombi ya mafao ya ukosefu wa ajira na dai langu linafanyiwa maamuzi, ila bado sijapata jibu kutoka kwao. Je, nitaweza kutuma maombi ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira pia?**

Hapana. Hauwezi kutuma maombi ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira ikiwa una maombi kwa sasa ambayo bado yanachakatuliwa kupitia maamuzi ya ukosefu wa ajira wa kawaida. Ikiwa umekataliwa mafao ya bima ya ukosefu wa ajira wa kawaida, unaweza kuwa na sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira lakini hautoweza kutuma maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira hadi pale uamuzi utakapochukuliwa.

**Je, nikikataa kurudi kazini pale nitakapoitwa na mwajiri wangu, kwasababu ninataka kupokea mafao ya ujumla ya ukosefu wa ajira, nitakuwa na sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Hapana. Kama ulikataa ajira inayofaa ili uweke maombi ya mafao ya ukosefu wa ajira, hautakuwa na sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Kupata taarifa zaidi, tembelea https://labor.vermont.gov/unemployment-insurance/refusal-return-work-covid-19

**Nina sifa ya ukosefu wa ajira wa kawaida lakini sikusanyi malipo kutokana na asilimia 100 ya tofauti. Je, nina sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**

Hapana. Kwenye kisa hiki, utakuwa na sifa ya kukusanya mafao ya kawaida ya ukosefu wa ajira pamoja na kupokea malipo hata pale yanapotumika kupunguza malipo yaliyopo yaliyopita kiasi. Hautakuwa na sifa ya ukosefu wa ajira wa kawaida wala Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Dai langu linasema kuwa liko katika malipo yaliyozidi kiasi na sipokei mafao ya serikali ya $600?**
Ikiwa dai lako lipo katika malipo yaliyozidi kiasi, Idara itahitaji kurekebisha dai lako ili kuweza kukuruhusu ukusanye mafao ya serikali ya $600. Tunayashughulikia madai haya. Unapaswa kuendelea kuweka madai ya wiki na punde dai lako litakapokuwa limerekebishwa, malipo yataanza kufanyika. Tafadhali zingatia kwamba, kiasi cha mafao yako ya wiki bado kitashikiliwa ili kiakisi tofauti ya salio lako la malipo yaliyozidi kiasi.

## MASWALI KUHUSU MAOMBI YA MSAADA WA JANGA LA UKOSEFU WA AJIRA

**Itakuwaje ikiwa nimemaliza maombi yangu ya awali ya mafao ya bima ya ukosefu wa ajira na nimepokea uamuzi wa kifedha wa $0? Je, nitahitaji kutuma tena maombi ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**
Ikiwa huna sifa ya kifedha ya ukosefu wa ajira wa kawaida, unaweza ukawa na sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira (PUA). Baada ya ukaguzi wa maombi yako kukamilika, Idara itakutaarifu kama unaweza kumaliza maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Je, ninaweza nikaacha katikati halafu nikaendelea baadaye kutuma maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**
Ndio. Ikiwa hujui jinsi ya kujibu swali, au unahitaji kuacha na kupata taarifa zaidi, unaweza kusitisha na kurudi baadae.

**Ninawezaje kurekebisha maombi yangu au thibitisho la dai langu la wiki ikiwa kwa bahati mbaya nimekosea kujibu swali ama nimeingiza taarifa zisizo sahihi?**
Unaweza kubadilisha namba zako za simu, anwani ya barua pepe, njia ya malipo, pamoja na kupakia nakala za kodi, unapomaliza kuweka thibitisho zako za dai la wiki. Wakati huu, hautaweza kubadili majibu

yaliyopo kwenye maombi yako. Majibu ya maswali mengine yanaweza kuhitaji madai yaingizwe kwenye mchakato wa ufanyaji maamuzi.

**Maombi yananiambia kwamba nambari yangu ya akaunti ya benki si sahihi. Nifanyeje?**
Ikiwa nambari ya akaunti yako ya benki inaanza ama inamalizika na sifuri, kuna dosari kwenye mfumo ambayo haikubali namba hizo za akaunti. Tunaposhuhulika kutatua tatizo hili, unaweza kuchagua kupokea cheki itakayotumwa kwako. Tatizo likishasuluhishwa, unaweza kurekebisha taarifa zako za malipo muda ujao utakapomaliza thibitisho lako la dai la wiki.

**Nilijaribu kuingia ili nimalize maombi yangu ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira na ninahitaji kutengeneza upya neno langu la siri, hata hivyo sijapata barua pepe ya jinsi ya kutengeneza nenosiri upya?**
Ikiwa unapokea hitilafu hii, tafadhali jaribu tena kutengeneza nenosiri upya kwani tatizo hili limekwisha fanyiwa suluhishi tangu 4/24/20. Ikiwa unajaribu kuingia ili kuweka dai lako la wiki la ukosefu wa ajira wa kawaida kwa kutumia nenosiri lako (PIN), hautoweza kuingia kwasababu hiyo ni tovuti tofauti.

**Nini kitatokea iwapo nitatoa taarifa za uongo ama za kupotosha ili nipate mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira?**
Utoaji taarifa za uongo ama zinazopotosha ili kupata mafao ni udanganyifu. Ukijulikana kuwa umefanya udanganyifu, utapewa faini na/ama kufunguliwa mashtaka ya jinai.

**Nilifuata maelekezo ya jinsi ya kumaliza maombi yangu ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Ninapata "Dai lisilostahiki. Dai lako la Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira limeonekana kuwa si stahiki kupokea mafao yoyote yajayo. Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali wasiliana na Idara ya Wafanyakazi ya Vermont kwenye (877) 660-7782." Nifanyeje?**

Umepokea barua pepe hii, kwasababu kutokana na majibu yako ya maswali yalioulizwa, umeonekana kuwa huna sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

**Nimemaliza maombi yangu ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira na nimeingiza taarifa zisizo sahihi za akaunti ya benki. Ninawezaje kurekebisha hili?**

Ikiwa unataka kurekebisha taarifa za akaunti yako ya benki, unaweza kubadili njia ya malipo wakati wa kuweka thibitisho lako la dai la wiki.

**Nilionekana kuwa sina sifa na ninataka kuomba rufaa ya uamuzi huu. Nifanyeje?**

Kama ulipokea uamuzi wa kuonekana kutokuwa na sifa, hutokuwa na sifa ya kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira. Ikiwa unahisi hili sio sawa, unaweza kuweka rufaa kwa kutuma faksi kwenda Kitengo cha Rufaa kwenye 802-828-4289 ama kutuma barua ya rufaa yako kwenda Idara ya Wafanyakazi kwenye S.L.P 488, Montpelier, VT 05601-0488. Kwenye rufaa yako, tafadhali weka: jina lako, jina la kampuni, pamoja na jina na tarehe ya nakala inayowekewa rufaa. Ombi lako la rufaa likishachakatuliwa, utapewa taarifa ya maandishi kuhusu tarehe na muda uliopangiwa kusikilizwa.

## MSAADA WA JANGA LA UKOSEFU WA AJIRA MASWALI KUHUSU NAKALA ZA KODI NA MISHAHARA ZINAZOTAKIWA

**Ninapaswa kupakia nakala zangu za kodi ndani ya siku 21. Muda huo wa siku 21 unaanza lini?**

Muda wa siku 21 unaanza pale unapomaliza maombi yako ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira, sio pale ulipotuma maombi ya awali ya ukosefu wa ajira.

**Wakati wa kuripoti mishahara kwenye maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira, natakiwa kuweka mshahara wa jumla ama mshahara unaopatikana baada ya kutoa matumizi?**
Watu waliojiajiri watapaswa kutumia mishahara yao ya baada ya kutoa matumizi. Wengine ambao hawajajiajiri watapaswa kuripoti mishahara yao ya JUMLA.

**Itakuwaje ikiwa ninalipwa kwa msingi wa komisheni au mauzo ninayofanya, sio kwa mshahara ama kwa lisaa?**
Ikiwa unalipwa kwa msingi wa komisheni au mauzo, unaweza kuingiza mishahara yako kwenye uwanja wa mshahara ama lisaa, ili mradi tu ziwe zinafanana na jumla ya mishahara iliyopatikana kwenye robo awamu.

**Ni nakala zipi za kodi zinazokubalika kuwekwa?**
Kipengele C, Kipengele E, Kipengele F: ikiwa umejiajiri ama ni mdau binafsi ambaye unawekwa kwenye Kipengele C, Kipengele E au Kipengele F, pamoja na kodi zako za mapato.

- 1040: Ikiwa unatumia kodi ya mapato ya 1040, ripoti mstari wa 1 wa mishahara kutoka kwenye mapato yako ya kodi (hii haijumuishi pensheni yoyote wala mapato ya ulinzi jamii)
- W2: ikiwa unatumia nakala ya kodi ya W2 kuripoti mishahara, ripoti mishahara iliyojumuishwa kwenye sanduku la 1 la tamshi la w2
- Je, itakuwaje ikiwa hawajakata kodi zangu za 2019 bado?

Ikiwa bado hujakata kodi zako za 2019 mpaka sasa, una siku 21 kufanya hivyo. Hata hivyo, utaweza kupokea kiasi cha chini cha mafao tu, hadi pale utakapoambatanisha nakala za uthibitisho.

**Kwanini ninahitajika kuweka nakala zangu za kodi za 2019 kama tarehe ya mwisho ya kukata kodi bado mpaka Julai 15?**
Nakala za kodi za 2019 zinahitajika kwasababu kiasi chako cha mafao kiko katika msingi wa mishahara iliyopatikana kwenye robo awamu 4

zilizopita. Kutoa mishahara ya 2019 kutasaidia kutambua kiasi fanisi cha mafao ya wiki. Ikiwa umeonekana kuwa na sifa ya kupata mafao, na haujatoa nakala ndani ya siku 21, utapokea kiasi cha chini cha mafao pekee, hadi pale utakapoweka nakala hizi. Una siku 21 za tangu ulipomaliza maombi yako ya awali ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira kuweka nakala hizi.

# MSAADA WA JANGA LA UKOSEFU WA AJIRA

# MASWALI KUHUSU MALIPO

**Je, kuna muda wa kusubiri kabla ya kupokea cheki yangu ya kwanza ya mafao?**
Hapana, hakuna muda wa chini wa kusubiri. Hatahivyo, kutegemeana na thibitisho zako za dai la wiki, inaweza kuchukua muda kukagua ama kufanya maamuzi ya dai lako.

**Kama nimejiajiri, lakini pia ninafanya kazi ya nusu muda kwa mwajiri mwingine. Kiasi cha mafao yangu ya wiki kitakuwaje?**
Ikiwa umeweka dai lako la Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira kama mtu aliyejiajiri, basi mishahara ya ajira yako pekee ndiyo itakayohesabiwa kwenye kiasi chako cha mafao ya wiki. Kama utaendelea kufanya kazi ya nusu muda, utapaswa kuripoti mishahara na masaa uliyofanya kazi kwenye kila thibitisho za dai la wiki.

**Je, nina sifa ya kupata mafao ya serikali ya $600/wiki ambayo wadai wengine wa UI wanapata?**
Ndio. Ikiwa una sifa za kupata Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira utakuwa una sifa pia ya kupata mafao ya $600/wiki. Hauhitaji kufanya chochote cha nyongeza, itajiingiza yenyewe kwenye malipo yako ya mafao ya wiki.

**Je, malipo hayo ya $600/wiki yatakuwa kwenye njia ile ile ya malipo au tofauti?**

Nyongeza ya mafao ya serikali ya $600 yataingizwa kwenye mfumo ule ule wa uingizaji wa moja kwa moja ama cheki kama ilivyo kwenye mafao yako ya wiki. Mafao haya ya serikali yanatozwa kodi za nchi pamoja na zile za kimataifa. Ikiwa ulichangua kodi zako kuzuiliwa, hili litajionyesha kwenye kiasi chako cha malipo. Ikiwa haukuchagua hivyo, utahitajika kuripoti hivyo utakapokuwa ukishughulikia kodi zako za mapato ya 2020.

**Kwanini sijapokea kiasi kamili cha mafao cha $600?**

Kipindi ulipomaliza maombi yako ya awali, kama ulichagua kodi zako kuzuiliwa kutoka kwenye kiasi chako cha mafao ya wiki, kodi zako zitazuiliwa pia kwenye mafao ya serikali ya $600. Mafao yote yanatozwa kodi za nchi pamoja na za serikali.

**Je, ninahitaji kuendelea kuweka madai ili kupata malipo yangu ya wiki?**

Ndio. Unahitajika kuweka dai kila wiki ambayo utahitaji kupokea mafao ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira.

- Unaweka madai ya wiki kwa ajili ya wiki iliyopita. (mfano. Kama umeweka dai la wiki siku ya Aprili 12, utakuwa umeweka dai la mafao ya wiki ya Aprili 5-11.) Unapofanya hivi, unakiri kuwa hukuajiriwa ama kuwa na kazi ya nusu muda katika wiki hiyo.
- Utapaswa kuweka dai la wiki kabla ya Ijumaa saa 4:00 jioni. (mfano., Kama ulikuwa haujaajiriwa katika wiki ya Aprili 5-11, unaweza kuweka dai kwanzia Aprili 12, lakini sio baada ya Aprili 17 saa 4jioni).
- Ni LAZIMA uripoti masaa uliyofanya kazi na mishahara ILIYOPATIKANA (bila kujali lini utalipwa) ikiwa ulifanya kazi katika wiki ambayo unaomba mafao. Kushindwa kufanya hivyo, kutatengeneza tatizo kwenye dai lako, kutachelewesha malipo yako, au kunaweza kukunyima sifa ya kupokea mafao.

**Je, nitapaswa kulipa kodi za nchi na za serikali kutoka kwenye mafao ninayopokea?**

Ndio. Wakati wa kuweka maombi, unapewa chaguzi ya kuzuiliwa kodi zako ama sivyo, hata hivyo mafao yote yanapaswa kulipiwa kodi za nchi na za serikali.

**Nitalipwa lini?**

Baada ya kumaliza maombi yako awali ya ukosefu wa ajira, maombi ya Msaada wa Janga la Ukosefu wa Ajira, na umeweka thibitisho lako la dai lako la kwanza la wiki, malipo yako yatachakatuliwa ndani ya siku 3 za biashara. Unaweza kuchagua njia ya malipo ya kuingiziwa pesa moja kwa moja ama cheki ya karatasi (njia ya kuingiziwa pesa moja kwa moja ni njia ya haraka zaidi).